# LEARNING BY EAR 2011

## “The Promised Land - A Story of African Migration to Europe”

## EPISODE TWELVE: “Asylum Granted, Asylum Denied”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Katrin Ogunsade, Klaus Dahmann**

**KISUAHELI: Eric Ponda**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: CHIVASI’S SHIP DOCKS AT A EUROPEAN PORT**

- **Chivasi (m, 22)**
- **Frontex guard (m, 40)**

**SCENE TWO: FLORENCE AND LINDA AT CHARLES' HOUSE**

- **Linda (f, 20)**
- **Florence (f, 35)**
- **Charles (m, 45)**

## SCENE THREE: CHIVASI AND FARAHANI MEET AT THE DETENTION CENTRE FOR ILLEGAL MIGRANTS

- **Chivasi (m, 22)**
- **Farahani (m, 19)**
- **Camp officer (m, 40)**
- **Immigration officer (m, 40)**

## INTRO:

Hujambo na karibu kwa makala nyingine ya Noa Bongo Jenga maisha yako. Hii ni sehemu ya 12 kwenye mfululizo wa mchezo huu wa redio **“Ardhi ya Ahadi kuhusu Waafrica wanaohamia Ulaya.”.** Farahani amekuwa kizuizini tangu kukamatwa kwake wiki mbili zilizopita kwa kujaribu kuhamia ulaya kinyume na sheria.Mazingira katika kizuizi hicho si mazuri. Na katika kipindi kilichotangulia Farahani anapanga mgomo wa kususia chakula. Yeye na pamoja na wahamiaji wengine haramu wanaamini kuwa hiyo ndiyo njia pekee ya kuwashinikiza maafisa nchi hiyo kuwapa hifadhi ya wakimbizi. Kwa upande mwengine Linda anayesomea uanasheria wa kimataifa amerejea Ulaya baada ya likizo fupi, na anafahamishwa kwamba maafisa wa uhamiaji wamekuwa wakimkimtembelea mumewe wa bandia  Charles. Zaidi ya hayo, Mamake Linda anampigia simu Linda kumfahamisha kwamba Babake amepata ajali na yuko hali mahututi hospitalini. Habari hizo zinamshtua sana Linda na kuzimia papo hapo. Huku hayo yakijiri,Mchumba wake Chivasi anajaribu kuhamia Ulaya kisiri ili aweze kuwa karibu na mpenzi wake.Amemlipa mlanguzi wa Watu ili aweze kufichwa kwenye meli ya Mizigo kutoka Ulaya. Je Chivasi atafanikiwa kufika Ardhi ya ahadi? Endelea kusikiliza kipindi cha leo. **Kupewa hifadhi, Kunyimwa hifadhi.** Na moja kwa moja tunaungana na Chivasi anapowasili bandari ya Ulaya alikowasili Farahani.

**SCENE ONE: CHIVASI'S SHIP DOCKS AT A EUROPEAN PORT**

1. **SFX: LOUD HOOT OF A SHIP ABOUT TO DOCK**

2. **FRONTEX GUARD:** **(orders)** Ni vyema kuigakua meli hii. Kwani imetoka Afrika kupeleka chakula cha msaada. Mlete huyo mbwa wa kunusa.

3. **SFX: DOGS SNIFFING**

4. **FRONTEX GUARD:** Wacha huyu mbwa akague haya masunduku.

5. **SFX: DOGS START BARKING LOUDLY**

6. **FRONTEX GUARD:** Hm…Hawa mbwa wameshuku kuna kitu hapa kwenye masanduku. Hebu yafungueni.

7. **SFX: WOODEN BOXES BEING RIPPED OPEN**

8. **FRONTEX GUARD:** **(shouts)** Hee kunawahamiaji haramu hapa! **(aside)** Hebu tokeni nje, tokeni.. tokeni.. pole pole. Musiwe na wasiwasi hatutamfanya chochote.
9. **CHIVASI:** **(hungry and thirsty)** Maji tafadhali.. Tafadhali nipeni maji.…

**10. FRONTEX GUARD: (orders)** Hebu mletee maji huyu! Haraka! Kisha chukua majina yao wote na tuwapeleke kizuizini mara moja..

**11. NARRATOR:** Chivasi na wahamiaji wengine wasio halali wanapewa maji na chakula. Kisha wanapelekwa moja kwa moja hadi katika kuzuizi anakozuiliwa rafiki yetu Farahani kutoka Africka kaskazini, ambako mafiasi wa uhamiaji wanajaribu kushughulikia ombi lake la kupewa hifadhi ya Ukimbizi. Kwa upande mwengine Linda amepata nafuu baada ya kuzimia. Rafiki yake Florence anajaribu kuhoji alichoambiwa na mamake kwenye simu..

**SCENE TWO: FLORENCE AND LINDA AT CHARLES' PLACE**

**12. FLORENCE:** Heee! Linda, umenishtua.

**13. LINDA:** Pole sana. Sikutarajia hivyo..! Ni babangu…?

**14. FLORENCE:** Babako anahitaji upasuaji wa dharura.Mamako ameniambia wanahitaji pesa haraka kugharamkia matibabu yake Hospitalini.

**15. LINDA:** Lakini pesa hizo nitazipata wapi? Ndio mwanzo nimerudi kutoka nyumbani. Nimetumia pesa zangu zote. Sina akiba yoyote sasa.

**16. FLORENCE:** Usijali- Nitakusaidia.

**17. LINDA:** **(excited)**Kweli? Ohh! Flo, ahsante sana! Nakushuru sana! Sijui nitakulipa vipi.

**18. FLORENCE:** Wacha kusoma ufanye kazi wakati wote kwenye klabu. Utapata pesa nyingi na kuwasaidia wazazi wako nyumbani.

**19. LINDA:** Lakini… lakini nahitaji kusomea shahada yangu ya digrii. Sitaweza kufanya hivyo…. ikiwa nitafanya kazi wakati wote au kwa masaa mengi.

**20. FLORENCE:** Linda, unaweza kuendelea na masomo yako baadaye. Lakini kazi yako…hmm, huwezi kujua. Hebu fikiria kwa muda mfupi umefanya kazi umepata pesa nyingi kugharamia mahitaji yako, na hata nauli ya kurudisha nyumbani. Sio wanafunzi wengi kutoka Afrika wanaoweza kufanya hivyo. Fikiria!.

**21. LINDA:** Flo, unaweza kumweleza Charles kwamba sitaweza kumlipa pesa zake mwezi huu kufungamana na mkataba wetu wa cheti cha Ndoa.? Samahani lakini lakini mambo ni mengi sana. Nilazima nitume pesa nyumbani kwa wazazi wangu. ,…. Na sijui nitafanyaje.

**22. FLORENCE:** **(calls out)** Charlie! Unaweza kufika hapa dakika moja?

**23. CHARLES:** Ndio,.. kuna nini?

**24. FLORENCE:** Linda hataweza kukulipa mwezi huu. Anahitajika

kutuma pesa nyumbani kugharamia matibabu ya upasuaji ya Babake.Lakini atakulipa mwezi ujao kama kawaida. Sivyo ulivyosema Linda?

**25. CHARLES:** **(unhappy)** Hii ni mara ya mwisho kufanya hivyo Florence. Sitarudia tena kufunga ndoa bandia.

**26. LINDA:** Eti nini…? **(PAUSE)** anasema nini? Kwani Charles ameoa hapo awali?

**27. FLORENCE:** Ndiyo ni mume wangu wa zamani!. Tulioana kwa miaka mitano, na sasa ndio wamiliki wa ile klabu unakofanya kazi, na tumewasaidia watu wengi sana kama wewe wanaohitaji vibali vya kufanya kazi Ulaya. Wewe ni watano sasa.

**28. LINDA:** **(bewildered)** Eti nini ?! Wacha utani!

**29. NARRATOR:** Hatimaye Linda ameanza kufahamu ukweli wa mambo,..sakata ambayo ameingizwa. Ni bahati tu kwamba sakata hii bado haijagunduliwa na maafisa wa uhamiaji.Je sakata hii itadumu kwa muda gani? Kwa upande mwengine katika kizuizi cha wahamiaji, Chivasi anafahamisha kuhusu sheria za nchi hiyo na kisha kupelekwa moja kwa moja hadi chumba atakamozuiliwa kwa muda usiojulikana. Na anakutana na wahamiaji wengine haramu miongoni mwao ni Farahani.

**<u>SCENE THREE: CHIVASI AND FARAHANI MEET AT THE DETENTION CENTRE FOR ILLEGAL MIGRANTS</u>**

**30. SFX: ELECTRIC BELL RINGING TO SIGNAL LUNCHTIME**

**31. CHIVASI:** Habari,,…? naitwa Chivasi Ja---

**32. FARAHANI:** Tosha !

**33. CHIVASI:** Samahani?

**34. FARAHANI:** Jina moja linatosha!. Naitwa Farahani. Hapa watu wanatumia jina moja hapa.

**35. CHIVASI:** Sawa naitwa Chivasi natoka…

**36. FARAHANI:** **(shocked)** Unawazimu wewe? Usithubutu hata kutaja nchi inayotoka!. Ni hatia kubwa hapa!. Usitaje Jina lako la pili au nchi unakotoka!

**37. CHIVASI:** Samahani sana. Sizifahamu viruzi sheria za hapa… Si hiyo ni kengele ya chakula cha mchana? Kwanini bado mumelala hapa.?

**38. FARAHANI:** Tumeanza mgomo wa kususia chakula.Tunataka wasikie kilio chetu na kukubali ombi letu la kupewa hifadhi kama wakimbizi. Wametufahamisha kwamba watawaleta maafisa wa uhamiaji hapa kusikiza maombi yetu. Kisha baadaye watakutana na jaji kuamua iwapo tunafaa kupewa hifadhi za wakimbizi.

**39. CHIVASI:** Lakini nilifikiri hapa Ulaya watu wanapewa makao, chakula, pesa na hifadhi kama mkimbizi moja kwa

moja kwa yoyote anayetaka.Sasa mtawaambia nini?.. Na je unafikiri watakubali ombi lenu?

**40. FARAHANI:** Itategemea!. Muhimu ni usibadili msimamo wako. Yaani leo uwambie hivi kesho vile. Watakurudisha haraka sana au kukuzuilia hapa kwa muda mrefu. Mimi napanga kuwaambia kwamba natoka nchi inayokumbwa na vita huko mashariki ya kati na ndio sababu nimetorokea Usalama wangu hapa Ulaya.

**41. CHIVASI:** Ahh ni sawa. Lakini ni kweli unatokea mashariki ya Kati?

**42. FARAHANI:** **(whispers)** Hiyo ni shida yangu na wala si yako.. Wewe jaribu kufikiria sabau itakayowashawishi. Watakuwa hapa wakati wowote kuanzia sasa.

**43. CHIVASI:** Lakini mimi sijatokea Mashariki ya kati! Ni wazi sifanani na watu wa huko. Je naweza kuwaambia kwamba natoroka umaskini na hali ya kukata tamaa ya maisha nchini mwangu?

**44. FARAHANI:** Sisi sote tuko hapa. Lakini sioni kama hiyo ni sababu ya kutosha itakayokuwezesha kupewa hifadhi kama mkimbizi.Pengine useme, kwa mfano umekuwa ukiteswa kutokana na imani yako ya kidini, au nchi yako inakumbwa na vita vya kikabila.

**45. CHIVASI:** Lakini … Nchini mwangu kuna amani!. Ingawa kumekuwa na ghasia za hapa na pale baada ya uchaguzi, na tatizo la ajira, lakini kawaida nchi yangu huwa na utulivu.

**46. FARAHANI:** Basi wewe hustali kuwa hapa. Kama huna shida kwanini ulihatarisha maisha yako kuja hapa?

**47. CHIVASI:** **(shy)** Kusema kweli nilifanya hivyo kumtafuta mchumba wangu hapa Ulaya. Nilikuwa nimemuahidi kwamba nitafanya kila niwezalo hata kama ni kuivuka bahari kudhihirisha pendo langu kwake.

**48. FARAHANI:** Eti nini?

**49. SFX: METAL BARRICADED DOOR OPENS**

**50. CAMP OFFICER:** Wewe – wewe uliwachochea wenzako kususia chakula. Njoo hapa. Hebu nifuate! Maafisa wa uhamiaji wanakusubiri. Na nyinyi wengine mnaweza kwenda kwa chakula chenu cha mchana mkitaka.

**51. CHIVASI:** Tafadhali , naomba kupiga simu ?

**52. CAMP OFFICER:** Wewe ni mgeni hapa na tayari unataka kupiga simu? Kumpigia nani? Rafiki yako ambaye pia amehamia hapa kinyume na sheria? Hapana hilo

haliwezekani. Utabaki hapa hadi pale utakapo tambuliwa kama mkimbizi humu nchini. Hapo utakuwa na uhuru wa kumpigia simu mtu yoyote utakaye.

**53. NARRATOR:** Ama kwa hakika Farahani anawaza sana! Anawaza jinsi atawashawishi maafisa wa uhamiaji kumpa hifadhi kama mkimbizi. Kwani anafahamu fika kwamba huu ndio wakati aliokuwa akisubiri kutimiza ndoto yake. Mambo ni mawili, kuishi Ulaya au kurejeshwa nyumbani. Hebu tusikilize mahojiano yake na maafisa wa uhamiaji.

**54. SFX: FILE BEING OPENED**

**55. IMM.OFFICER:** Ehhe, kijana unataka kupewa hifadhi kama mkimbizi.Unaweza kunieleza kwanini ?

**56. FARAHANI:** Najihisi kuwa niko salama sana hapa. Nimekuwa nikikwepa risasi kukimbilia usalama wangu, lakini hatimaye hapa naweza kupata usingizi na amani?

**57. IMM.OFFICER:** Umekuwa ukikwepa risasi? Kutoka kwa kina nani? Na wapi huko?

**58. FARAHANI:** **(hesitant)** Nchini mwangu sijashuhudia amani. Serikali imekuwa ikikabiliana na makundi ya wapiganaji kwa muda mrefu. Na watu wengi hasa kutoka familia yangu wameuawa kwenye mapigano hayo.

**59. IMM.OFFICER:** Unasema umetokea Mashariki ya Kati. Sivyo?

**60. FARAHANI:** Ndio.

**61. IMM.OFFICER:** Unazunguma Kiarabu?

**62. FARAHANI:** Ndio, hiyo ndio lugha mama. Shuleni nilisoma Kiingereza lakini nikiwa nyumbani na wazazi wangu nazungumza Kiarabu.

**63. IMM. OFFICER:** Hmm. Nitawauliza mwenzangu kuja kuzungumza nawe baadaye.Yeye anatoka Mashariki ya kati na anazungumza vizuri lugha hiyo ya Kirabu.Ataweza kutofautisha fasaha yako.

**64. FARAHANI:** Sawa hakuna shida.

**65. IMM. OFFICER:** Sasa hapa ulifika vipi? Hapa Ulaya, sio katika jela hii..

**66. FARAHANI:** Tulitoroka vita nchini mwangu niliko zaliwa na kutembea kwa miguu kwa siku kadhaa hadi nilipokutana na msamaria mwema aliyetupeleka hadi Afrika kaskazini. Kufika huko tlilazimika kulipia mashua iliyotupeleka hadi hapa Ulaya. Lakini tulipokuwa karibu kufika ufuoni, alitwambia tuogelee hadi ufuoni kwa kuwa hawezi kufika .. Niliogelea hadi nilipookolewa na maafisa wa usalama wanashika doria baharini ambao walinileta hapa.

**67. SFX: SCRIBBLING ON PAPER**

**68. IMM. OFFICER:** Hmm. Huyu lazima atakuwa miongoni mwa wale waliopatikana baharini wiki chache zilizopita. Nilisikia kuhusu habari hizo. Na watu wengine 20 walikufa maji. Sivyo?

**69. FARAHANI:** Ndio. Ni wacache wetu tu tulionusurika.

**70. IMM. OFFICER**: Sawa nimesiki hadithi yako. Hii ni mwanzo tu wa mahojiano yatakayo endelea.Mwenzangu atakuja baadaye kukuhoji zaidi. Kumbuka! Tukigundua kwamba unadanganya, basi ombi lako la kutaka kupewa hifadhi kama mkimbizi litatupiliwa mbali na kurejeshwa ulikotoka. Ni hayo tu kwa sasa. **(calls out)** mwengine tafadhali!

**OUTRO:**

Mmoja baada ya mwengine wahamiaji hao walielezea hadithi zao, nyingi za ukweli nyingine za urongo na jinsi walivyotoroka makwao kufika Ulaya. Chivasi atakuwa wa mwisho kuitwa. Je atakuwa na hadithi gani? Ungana nasi usikie yatakayojiri.

Ukitaka unaweza kuungana nasi kwa mjadala wazi kwenye ukurasa wetu wa Facebook **dw-de/destinationeurope**. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.